
BARAZA LA TAIFA LA HUDUMA JUMUISHI
ZA FEDHA TANZANIA




# MTAALA WA WAELIMISHAJI WALIOTHIBITISHWA WA ELIMU YA FEDHA

© BARAZA LA TAIFA LA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA TANZANIA 2023



# YALIOMO

UMUHIMU NA MALENGO YA PROGRAMU YA WAELIMISHAJI WALIOTHIBITISHWA WA ELIMU YA FEDHA. .......... 1
VIGEZO VYA UANDIKISHAJI .......... 2
MUUNDO WA PROGRAMU .......... 3
TATHMINI .......... 3
KIWANGO CHA HADIA KINACHOHITAJIKA .......... 4
MISIMBO YA MODULI .......... 4
MFUMO WA KUWEKA MADARAJA .......... 5
MODULI ZA PROGRAMU .......... 5
MAELEZO YA MTAALA .......... 7
MATOKEO MAKUU YA UJIFUNZAJI, HADIA NA VIGEZO VYA TATHMINI .......... 8
VIWANGO NA MATOKEO WEZESHI .......... 9
MATOKEO MADOGO WEZESHI .......... 9
VIGEZO VYA TATHMINI NA VIWANGO VYAKE .......... 11
MAELEZO YA MODULI .......... 23
WADAU WA MSINGI .......... 28
MAREJELEO .......... 29

Mtaala huu umetolewa chini ya Mpango Mkakati wa tatu wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha (2023 – 2028) ili kutekeleza Mwongozo wa Taifa wa Waelimishaji wa Elimu ya Fedha uliotolewa Julai 2023. Moduli za mtaala huu zitasaidia kujenga uwezo wa usimamizi binafsi wa fedha kwa watu walio nje ya mfumo rasmi wa elimu katika kutumia bidhaa na huduma za fedha, pamoja na kujihusisha na watoa huduma za fedha na wasimamizi wa sekta ya fedha.

1

# UMUHIMU NA MALENGO YA PROGRAMU YA WAELIMISHAJI WALIOTHIBITISHWA

Sehemu hii inaelezea umuhimu na malengo ya Programu ya Waelimishaji Waliothibitishwa wa Elimu ya Fedha.

## Utangulizi

Elimu na ustadi wa fedha una mchango mkubwa katika huduma jumuishi za fedha na uthabiti wa sekta ya fedha, hii inachochea ukuaji endelevu wa uchumi kwa kuwawezesha watu kuwa na uwezo wa usimamizi binafsi wa fedha. Licha ya mchango huo muhimu, viwango vya uelewa wa kifedha kwa watu walio nje ya mfumo rasmi wa elimu nchini bado viko chini. Hali hii inachangiwa na upungufu wa mikakati inayoweza kubadilisha tabia, zinazojikita zaidi katika maeneo ya mijini, na hutolewa kwa njia isiyo na mfumo maalum na isiyokuwa na viwango.

Kwa msingi huu, Benki Kuu ya Tanzania, katika mamlaka yake ya kuhamasisha huduma jumuishi za fedha, kuhakikisha uadilifu na uthabiti wa mfumo wa fedha, na kama Sekretarieti ya Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Fedha, imeendelea kutatua changamoto za ujuzi wa masuala ya fedha kwa watu walio nje ya mfumo rasmi wa elimu. Aidha, Benki Kuu inatekeleza Mwongozo wa Taifa wa Waelimishaji wa Elimu Fedha, kwa kuandaa na kutekeleza mtaala huu wa Mwelimishaji Aliyethibitishwa wa Elimu ya Fedha.

Mtaala huu utatekelezwa kupitia taasisi za elimu, mafunzo na utaalamu zilizoainishwa na Benki Kuu ya Tanzania, zenye ujuzi na maarifa ya elimu na ustadi wa masuala ya kifedha.

## Umuhimu

Hii ni programu inayolenga kumpa ujuzi Mwelimishaji wa Elimu ya Fedha utakaomwezesha kutekeleza jukumu lolote kuhusu elimu ya fedha.

### Madhumuni

Madhumuni ya programu hii ni kuwaandaa Waelimishaji wa Elimu ya Fedha wenye umahiri, ujuzi na weledi ambao watatoa elimu na ustadi wa masuala ya kifedha ili kuuwezesha umma kuwa na ujuzi huo.

### Malengo

Lengo kuu la programu hii ni kuhakikisha utoaji wa ujuzi wa masuala ya fedha kwa umma unakuwa wa utaratibu maalum, wenye ufanisi, na endelevu. Hivyo, programu hii itahakikisha ulinganifu katika utoaji wa elimu ya fedha pamoja na utumiaji sahihi wa rasilimali katika kutatua changamoto ya uelewa mdogo wa masuala ya kifedha kwa watu walio nje ya mfumo rasmi wa elimu.
Malengo mahususi ya programu hii ni:

a. kuwajengea waelimishaji wa elimu ya masuala ya kifedha nchini uwezo wa kuwasilisha ujuzi wa usimamizi binafsi wa fedha kwa umma;

b. kujenga ulinganifu katika utoaji elimu ya masuala ya kifedha kwa umma;

c. kuwa na kanzidata ya waelimishaji wa elimu ya masuala ya kifedha waliopatiwa mafunzo;

d. kusimamia mienendo ya waelimishaji wa elimu ya masuala kifedha waliopatiwa mafunzo; na

e. kuwa na matumizi sahihi ya rasilimali kwa kutoa mafunzo kwa wahamasishaji na watu walioteuliwa kutoa elimu ya masuala ya kifedha kwa umma.

# 2 VIGEZO VYA UANDIKISHAJI

Programu ya Waelimishaji Waliothibitishwa wa Elimu ya Fedha inawalenga waombaji wanaotoa au wanaokusudia kutoa elimu ya masuala ya kifedha kwa umma. Waombaji wanaweza kuwa watu binafsi, wanaoshirikiana na wasimamizi wa sekta ya fedha, kampuni, taasisi za serikali, taasisi za umma, vikundi vya kijamii, asasi za kiraia na asasi zisizo za serikali, na watoa huduma wengine wa sekta binafsi na za umma. Kigezo cha chini cha kujiunga na programu hii ni Cheti cha Kidato cha Nne.

# 3 MUUNDO WA PROGRAMU

Programu hii inajumuisha moduli tano (5), ambazo zitafundishwa kwa muda wa siku kumi (10) za kazi kwa utaratibu wa masomo ya kutwa, au siku ishirini (20) za kazi kwa utaratibu wa masomo ya jioni. Ili kuimarisha uwasilishaji wa stadi muhimu zinazohitajika kwa waelimishaji wa elimu ya fedha, mkufunzi mwalikwa au mhamasishaji ataalikwa kutoa wasilisho kuhusu ujuzi wa mawasiliano na uwasilishaji wa mada kwa muda usiopungua saa tatu, pamoja na utoaji wa tathmini endelevu.

# 4 TATHMINI

Tathmini ni sehemu muhimu ya mchakato wa ujifunzaji na inapaswa kuwezesha na kukamilisha mikakati ya ujifunzaji ili kufikia matokeo yanayokusudiwa. Kimsingi, tathmini inapaswa kuakisi maendeleo yanayotarajiwa na kuzingatia ujuzi mbalimbaili uliotolewa.

## Misingi ya Tathmini

a. Tathmini itaakisi madhumuni na malengo ya programu nzima, mbinu za mafunzo na matokeo ya ujifunzaji wa moduli.

b. Tathmini itaundwa kusaidia mafunzo ya waelimishaji wa elimu ya fedha, haswa maendeleo yao kama Wanafunzi wanaojiongoza katika kupata ujuzi muhimu.

c. Tathmini zitafanyika kwa namna mbalimbali, ili kutoa motisha kwa waelimishaji wa elimu ya fedha na kutambua mbinu za ujifunzaji zitakazowawezesha waelimishaji wa elimu ya masuala ya kifedha kuonesha kwamba wamefikia malengo ya kujifunza.

d. Tathmini itaakisi maendeleo katika kipindi cha ujifunzaji, pamoja na ongezeko la mbinu changamano zinazohusishwa na ujuzi wa juu zaidi.

### Mbinu za Tathmini

Mbinu zifuatazo za tathmini zitatumika:

### Tathmini Endelevu

Lengo la tathmini endelevu ni kuimarisha mchakato wa ujifunzaji kwa kuhusisha ushiriki wa waelimishaji katika kuwasilisha ujuzi wa elimu ya masuala ya kifedha kwa umma. Tathmini endelevu itachangia asilimia 60 ya kila moduli. Utoaji wa alama kwa kazi binafsi utakuwa asilimia 20 na kazi ya kikundi itakuwa asilimia 30 kwa kila moduli, wakati video moja ya dakika kumi iliyorekodiwa ya kipindi cha mafunzo ya vitendo itakuwa na jumla ya asilimia 50 kwa tathmini endelevu ya programu nzima, ikigawanywa kama asilimia 10 ya tathmini endelevu kwa kila moduli.

### Mtihani wa Mwisho wa Programu

Kutakuwa na mtihani wa jumla utakaohusisha maswali kutoka kwenye moduli tano (5), ambapo idadi na ugawanywaji wa maswali utalingana na uzito wa hadia kwa kila moduli. Mtihani huu utafanyika kwa muda usiopungua saa mbili (2). Mtihani huo utajumuisha maswali funge, mfano maswali ya kuchagua au maswali ya ndiyo/hapana. Utaratibu wa usimamizi utazingatiwa wakati wa kufanya mtihani. Mtihani huu utachangia asilimia 40 ya tathmini, itakayogawanywa kwa kila tathmini ya mwisho ya moduli kulingana na idadi ya maswali na uzito wa hadia.

## 5 KIWANGO CHA HADIA KINACHOHITAJIKA

Programu hii ina moduli 5, ambazo zina jumla ya hadia 8.

# 6 MISIMBO YA MODULI

Mfumo wa misimbo umejumuisha herufi na tarakimu, ambazo zina maana maalum. Kwa mfano, moduli ifuatayo;

| | |
|---|---|
| CFE01 | Inawakilisha Ujuzi wa Hesabu za Fedha |
| CFE | Inawakilisha Mwelimishaji Aliyethibitishwa wa Elimu ya Fedha |
| 01 | Inawakilisha moduli ya kwanza ya programu |

# 7 MFUMO WA KUWEKA MADARAJA

Alama zitatolewa chini ya asilimia 100. Alama zilizopatikana kutokana na tathmini mbalimbali zitapangwa kama ifuatavyo:

| Alama (%) | 80-100 | 60-79 | 50 - 59 | 40-49 | 0-39 |
|---|---|---|---|---|---|
| Daraja | A | B+ | B | C | D |
| Maoni | Bora | Vizuri Sana | Vizuri | Inaridhisha | Dhaifu |

Cheti kitatolewa kwa mwelimishaji ambaye atatimiza masharti yafuatayo:

a. Awe amekamilisha moduli zote; na

b. Awe amefikia kiwango cha chini cha wastani wa B.

# 8 MODULI ZA PROGRAMU

## Hadia za moduli

Jedwali hili linaeleza moduli za masomo kwa kuonesha mpango wa masomo na hadia kwa kila moduli

| Msimbo | Jina | Mpango wa Masomo (Saa kwa Wiki) | | | | Hadia za moduli |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | M | MA | MV | MM | |
| CFE01 | Ujuzi wa Hesabu za Kifedha | 5 | 2.75 | 2:00 | 0.25 | 1 |
| CFE02 | Mfumo wa Ikolojia ya Kifedha | 5 | 2:50 | 2:00 | 0.50 | 1 |
| CFE03 | Usimamizi wa Fedha | 15 | 8:50 | 6:00 | 0.50 | 3 |
| CFE04 | Majukumu ya Kifedha | 5 | 2.75 | 2:00 | 0.25 | 1 |
| CFE05 | Ulinzi Binafsi wa Kifedha | 10 | 5:50 | 4:00 | 0.50 | 2 |
| Jumla Ndogo | | | | | | 8 |

Ufunguo: M. Mhadhara; MA. Mazoezi; MV. Mafunzo kwa Vitendo; MM… Mtihani wa Mwisho

## Muhtasari wa Moduli

Jedwali hili linaeleza moduli na wiki ambayo masomo husika yatafundishwa.

| Na. | Msimbo | Jina | Wiki | |
|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 |
| 1 | CFE01 | Ujuzi wa Hesabu za Kifedha | √ | |
| 2 | CFE02 | Mfumo wa Ikolojia ya Kifedha | √ | |
| 3 | CFE03 | Usimamizi wa Fedha | √ | |
| 4 | CFE04 | Majukumu ya Kifedha | | √ |
| 5 | CFE05 | Ulinzi Binafsi wa Kifedha | | √ |

# 9 MAELEZO YA MTAALA

| Na. | Sifa ya Mhitimu | Mwelimishaji Aliyethibitishwa wa Elimu ya Fedha |
|---|---|---|
| 1 | Madhumuni | Hii ni programu inayolenga kumpa ujuzi Mwelimishaji wa Elimu ya Fedha utakaomwezesha kutekeleza jukumu lolote kuhusu elimu ya fedha. |
| 2 | Umahiri | Programu hii inathibitisha wahitimu ili waweze kutumia maarifa, ujuzi, na umahiri katika fani mahususi kwa taratibu zilizothibitishwa. |
| 3 | Hadia | 8 |
| 4 | Jumla ya hadia kutoka daraja la chini zaidi: | - |
| 5 | Jumla ya hadia | 8 |
| 6 | Tarehe ya mwisho ya mapitio ya mtaala | 24 Novemba 2023 |
| 7 | Vigezo vya uandikishaji | Programu ya Waelimishaji Waliothibitishwa wa Elimu ya Fedha inawalenga waombaji wanaotoa au wanaokusudia kutoa elimu ya masuala ya kifedha kwa umma. Waombaji wanaweza kuwa watu binafsi, wanaoshirikiana na wasimamizi wa sekta ya fedha, kampuni, taasisi za serikali, taasisi za umma, vikundi vya kijamii, asasi za kiraia na asasi zisizo za serikali, na watoa huduma wengine wa sekta binafsi na za umma. Kigezo cha chini cha kujiunga na programu hii ni Cheti cha Kidato cha Nne. |

# 10 MATOKEO MAKUU YA UJIFUNZAJI, HADIA NA VIGEZO VYA TATHMINI

| **Matokeo Makuu ya Ujifunzaji**<br>**Wanafunzi wataweza;** | | **HADIA** | **Vigezo vya Tathmini**<br>**Wanafunzi wanapaswa;** |
|---|---|---|---|
| 1 | kutumia ujuzi wa hesabu za kifedha na maarifa kuhusu mfumo wa ikolojia ya kifedha kwa ajili ya usimamizi binafsi wa fedha. | 2 | a) kutumia ujuzi wa hesabu za kifedha katika kufanya uamuzi binafsi wa masuala ya kifedha. |
| | | | b) kuelezea mfumo wa ikolojia ya kifedha kuhusiana na watoa huduma, bidhaa na huduma, mazingira ya udhibiti wa kifedha na miundombinu wezeshi. |
| 2 | kutumia ujuzi wa usimamizi wa fedha kwa ajili ya usimamizi binafsi wa fedha. | 3 | a) kutumia ujuzi wa usimamizi wa fedha katika masuala binafsi ya fedha. |
| 3 | kutumia ujuzi katika kutimiza majukumu ya kifedha na ulinzi binafsi wa kifedha kwa ajili ya usimamizi binafsi wa fedha. | 3 | a) kuelezea majukumu ya kifedha yanayohusiana na masuala binafsi ya fedha.<br><br>b) kuchanganua ulinzi binafsi wa kifedha unaohusiana na uamuzi binafsi wa masuala ya kifedha. |
| | | | |
| JUMLA | | 8 | |

# 11 VIWANGO NA MATOKEO WEZESHI

| Matokeo Makuu ya Ujifunzaji<br>**Wanafunzi wataweza;** | Matokeo Wezeshi<br>**Wanafunzi wataweza;** |
|---|---|
| 1. kutumia ujuzi wa hesabu za kifedha na maarifa kuhusu mfumo wa ikolojia ya kifedha kwa ajili ya usimamizi binafsi wa fedha. | 1.1 kutumia ujuzi wa hesabu za kifedha katika kufanya uamuzi binafsi wa masuala ya kifedha.<br>1.2 kuelezea mfumo wa ikolojia ya kifedha kuhusiana na watoa huduma, bidhaa na huduma, mazingira ya udhibiti wa kifedha na miundombinu wezeshi. |
| 2. kutumia ujuzi wa usimamizi wa fedha kwa ajili ya usimamizi binafsi wa fedha. | 2.1 kutumia ujuzi wa usimamizi wa fedha katika masuala binafsi ya fedha. |
| 3. kutumia ujuzi katika kutimiza majukumu ya kifedha na ulinzi binafsi wa kifedha kwa ajili ya usimamizi binafsi wa fedha. | 3.1 kuelezea majukumu ya kifedha yanayohusiana na masuala binafsi ya fedha.<br>3.2 kuchanganua ulinzi binafsi wa kifedha unaohusiana na uamuzi binafsi wa masuala ya kifedha. |

# 12 MATOKEO MADOGO WEZESHI

| Matokeo Wezeshi<br>**Wanafunzi wataweza;** | Matokeo Madogo Wezeshi<br>**Wanafunzi wataweza;** |
|---|---|
| 1.1 kutumia ujuzi wa hesabu za kifedha katika kufanya uamuzi binafsi wa masuala ya kifedha. | 1.1.1 kuonesha ujuzi wa msingi wa hesabu katika masuala binafsi ya fedha. |
| | 1.1.2 kukokotoa viwango vya riba kwenye bidhaa na huduma za fedha. |
| | 1.1.3 Kutumia ujuzi wa hesabu za kifedha kwa ajili ya kufanya uamuzi wa kifedha. |
| 1.2 kuelezea mfumo wa ikolojia ya kifedha kuhusiana na watoa huduma, bidhaa na huduma, mazingira ya udhibiti wa kifedha na miundombinu wezeshi | 1.2.1 kuelezea kuhusu watoa huduma za fedha kwa masuala binafsi ya kifedha |

| | |
|---|---|
| | 1.2.2 kuelezea kuhusu bidhaa na huduma za fedha kwa masuala binafsi ya kifedha |
| | 1.2.3 kuonesha mazingira ya kisheria na usimamizi kwa ajili ya masuala binafsi ya kifedha. |
| | 1.2.4 kuonesha miundombinu wezeshi ya kupata huduma za kifedha kwa ajili ya masuala binafsi ya kifedha |
| 2.1 kutumia ujuzi wa usimamizi wa fedha katika masuala binafsi ya fedha. | 2.1.1 kutofautisha fedha halali na fedha bandia. |
| | 2.1.2 kuchambua mchakato wa fedha zenye ubora kama unavyotumika katika usimamizi wa fedha |
| | 2.1.3 kuelezea shughuli halali za kuzalisha mapato na maadili ya kazi kulingana na sheria za nchi. |
| | 2.1.4 kuchambua mchakato wa kuweka akiba kama ilivyo katika usimamizi wa fedha. |
| | 2.1.5 kuandaa bajeti na mpango binafsi wa fedha kama ilivyo katika usimamizi wa fedha. |
| | 2.1.6 kuchambua mchakato wa kukopa kama unavyotumika katika usimamizi binafsi wa fedha |
| 3.1 kuelezea majukumu ya kifedha yanayohusiana na masuala binafsi ya fedha. | 3.1.1 kuelezea wajibu binafsi katika kodi unaohusiana na masuala binafsi ya kifedha |
| | 3.1.2 kuelezea wajibu wa kifedha unaohusiana na usimamizi binafsi wa fedha |
| | 3.1.3 kuelezea shughuli haramu za kifedha zinazohusiana na usimamizi binafsi wa fedha |
| 3.2 kuchanganua ulinzi binafsi wa kifedha unaohusiana na uamuzi binafsi wa masuala ya kifedha | 3.2.1 kuchambua mchakato wa udhibiti wa vihatarishi vya masuala binafsi ya fedha. |
| | 3.2.2 kuchambua mchakato wa mipango ya muda mrefu ya masuala binafsi ya kifedha |
| | 3.2.3 kuelezea mchakato wa kuwalinda watumiaji wa huduma za kifedha kama unavyotumika katika masuala binafsi ya kifedha |

# 13 VIGEZO VYA TATHMINI NA VIWANGO VYAKE

## Vigezo na Nyenzo za Tathmini

| Matokeo Madogo Wezeshi<br>**Wanafunzi wataweza;** | Shughuli zinazofanyika |
|---|---|
| 1.1.1. kuonesha ujuzi wa msingi wa hesabu katika masuala binafsi ya fedha. | kuonesha aina za hesabu za msingi za kifedha. |
| | kufanya uwiano rahisi na uchambuzi wa mwenendo wa kifedha unaohusiana na masuala binafsi ya kifedha. |
| | kutafsiri matokeo ya uwiano rahisi na uchambuzi wa mwenendo wa kifedha unaohusiana na masuala binafsi ya kifedha. |
| 1.1.2. kukokotoa viwango vya riba kwenye bidhaa na huduma za fedha. | kuelezea aina tofauti za viwango vya riba za bidhaa na huduma za kifedha. |
| | kuelezea dhana ya thamani ya fedha kulingana na wakati |
| | kufanya hesabu rahisi za punguzo na ongezeko la thamani ya fedha kulingana na wakati |
| | Kukokotoa kiwango cha riba kwenye bidhaa na huduma za kifedha. |
| | Kutafsiri maana ya viwango vya riba vilivyokokotolewa kwenye bidhaa na huduma za kifedha. |
| 1.1.3. Kutumia ujuzi wa hesabu za kifedha kwa ajili ya kufanya uamuzi wa kifedha. | kuelezea dhana za hesabu katika mipango ya kifedha. |
| | kuelezea dhana mbalimbali za hesabu katika mipango ya kifedha. |
| | kutafsiri taarifa za hesabu kwa ajili ya kufanya uamuzi wa masuala ya kifedha. |
| 1.2.1. kuelezea kuhusu watoa huduma za fedha kwa masuala binafsi ya kifedha | kuelezea aina mbalimbali za watoa huduma za fedha. |
| | kuelezea faida na hasara za watoa huduma mbalimbali za kifedha. |
| | Kuelezea mahitaji kwa ajili ya kupata huduma kutoka kwa watoa huduma za kifedha. |

| | Vigezo vya tathmini | Mbinu za tathmini | Nyenzo za tathmini |
|---|---|---|---|
| | 1.1.1.1. kuonesha kwa usahihi ujuzi wa msingi wa hesabu katika masuala binafsi ya fedha. | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 1.1.2.1. kukokotoa kwa usahihi viwango vya riba kwenye bidhaa na huduma za kifedha | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 1.1.3.1. kutumia kwa usahihi stadi za hesabu kwa ajili ya kufanya uamuzi wa masuala ya kifedha | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 1.2.1.1. kuelezea kwa usahihi watoa huduma za fedha | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |

| Matokeo Madogo Wezeshi<br>**Wanafunzi wataweza;** | Shughuli zinazofanyika |
|---|---|
| 1.2.2. kuelezea bidhaa na huduma za fedha kwa masuala binafsi ya kifedha | kuelezea aina mbalimbali za bidhaa na huduma za fedha. |
| | kuelezea faida na hasara za bidhaa na huduma mbalimbali za fedha. |
| | kufafanua njia mbalimbali za utoaji wa bidhaa na huduma za fedha (njia halisi na za kidijiti). |
| 1.2.3. kuonesha mazingira ya kisheria na usimamizi kwa ajili ya masuala binafsi ya kifedha | kuelezea mamlaka tofauti za usimamizi wa fedha na mawanda yake. |
| | kutoa mifano ya vyombo vya kisheria na usimamizi wa masuala binafsi ya kifedha. |
| | kuonesha namna ya kushirikiana na mamlaka za usimamizi. |
| 1.2.4.. kuonesha miundombinu wezeshi ya kupata huduma za kifedha kwa ajili ya masuala binafsi ya kifedha. | kuelezea mifumo ya malipo, bidhaa na huduma za fedha |
| | kuelezea umuhimu wa kuandika na kuhifadhi nyaraka katika kupata huduma za fedha. |
| | kuonesha mifano ya dhamana mbalimbali ili kupata bidhaa na huduma za fedha |
| | kuelezea miundombinu ya taarifa inayowezesha kufanya tathmini ya huduma za mikopo. |
| | Kuelezea umuhimu wa ufuatiliaji wa taarifa za fedha kidijiti katika kuongeza upatikanaji wa fedha kwa watu binafsi. |
| | kuelezea miundombinu inayowezesha utoaji wa bidhaa na huduma za fedha. |
| 2.1.1. kutofautisha fedha halali na fedha bandia. | kufafanua fedha halali na bandia. |
| | kueleza alama za utambuzi wa fedha halali. |
| | kutambua fedha halali na bandia. |
| | kutumia zana na vifaa katika kutambua fedha halali. |

| | Vigezo vya tathmini | Mbinu za tathmini | Nyenzo za tathmini |
|---|---|---|---|
| | 1.2.2.1. kuelezea kwa usahihi bidhaa na huduma za fedha. | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 1.2.3.1. kuelezea kwa usahihi mazingira ya kisheria na usimamizi. | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 1.2.4.1 kuelezea kwa usahihi miundombinu wezeshi ya kupata huduma za fedha kwa masuala binafsi ya kifedha. | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 2.1.1.1 kuelezea kwa usahihi tofauti kati ya fedha halali na bandia. | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |

| **Matokeo Madogo Wezeshi**<br>**Wanafunzi wataweza;** | **Shughuli zinazofanyika** |
|---|---|
| 2.1.2. kuchambua mchakato wa fedha zenye ubora kama inavyotumika katika usimamizi wa fedha. | kufafanua fedha zenye ubora. |
| | kuelezea sifa za fedha zenye ubora. |
| | kuonesha njia sahihi za kutumia na kutunza fedha. |
| | kuelezea hatua za kushughulikia fedha zilizoharibika. |
| 2.1.3. kuelezea shughuli halali za kuzalisha mapato na maadili ya kazi kulingana na sheria za nchi. | kutambua shughuli halali za kuzalisha mapato katika uchumi. |
| | kutambua fursa za shughuli halali za kuzalisha mapato. |
| | kuhusianisha fursa za shughuli halali za kuzalisha mapato na maadili ya kazi. |
| 2.1.4. kuchambua mchakato wa kuweka akiba kama ilivyo katika usimamizi wa fedha | kuelezea umuhimu wa kuweka akiba. |
| | kuelezea njia/mbinu tofauti za kuweka akiba . |
| | kufafanua huduma mbali mbali za kuweka akiba zinazopatikana na faida/hasara zake. |
| 2.1.5. kuandaa bajeti na mpango binafsi wa fedha kama ilivyo katika usimamizi wa fedha. | kuelezea umuhimu wa bajeti na mipango. |
| | kuhusianisha bajeti, mipango na malengo binafsi. |
| | kuonesha mgawanyo wa makundi ya mapato na matumizi yanayohusiana na shughuli mbalimbali katika usimamizi wa fedha. |
| | kufuatilia mapato na matumizi kwa ajili ya kufanya uamuzi wa mipango binafsi ya kifedha |
| | kuonesha zana za teknolojia ya kifedha kwa ajili ya mipango na bajeti |
| | kuelezea umuhimu wa bajeti na mipango. |

| | Vigezo vya tathmini | Mbinu za tathmini | Nyenzo za tathmini |
|---|---|---|---|
| | 2.1.2.1 kuchambua kwa usahihi mchakato wa fedha zenye ubora kama inavyotumika katika usimamizi wa fedha. | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 2.1.3.1 kuelezea kwa usahihi shughuli halali za kuzalisha mapato na maadili ya kazi kwa mujibu wa sheria za nchi . | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 2.1.4.1 kuchambua kwa usahihi mchakato wa kuweka akiba kama unavyotumika katika usimamizi wa fedha. | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 2.1.5.1. kuelezea kwa usahihi bajeti na mchakato wa mipango ya fedha kama inavyotumika katika usimamizi wa fedha | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |

| **Matokeo Madogo Wezeshi**<br><br>**Wanafunzi wataweza;** | **Shughuli zinazofanyika** |
|---|---|
| 2.1.6. kuchambua mchakato wa kukopa kama unavyotumika katika usimamizi binafsi wa fedha | kuelezea umuhimu na sababu za ukopaji. |
| | kuelezea sifa za kukopa kwa uwajibikaji ili kuepuka kuwa na mlundikano wa madeni |
| | kuelezea njia zinazofaa za ukopaji. |
| | kubainisha vipengele muhimu vya vigezo na masharti (viwango vya riba, awamu za malipo, adhabu/tozo, muda wa malipo, n.k.) yanayohusiana na ukopaji. |
| | kuelezea uhitaji wa taarifa za wakopaji katika mifumo ya kumbukumbu za mikopo. |
| | Kuonesha athari ya kushindwa kulipa mikopo |
| 3.1.1. kuelezea wajibu binafsi katika kodi unaohusiana na masuala binafsi ya kifedha | kuelezea umuhimu na faida za kulipa kodi katika uchumi. |
| | kuelezea aina mbalimbali za kodi zinazohusiana na usimamizi binafsi wa fedha. |
| | kufafanua haki na majukumu katika utekelezaji wa kanuni za kodi |
| | kuelezea madhara ya kukiuka sheria na kanuni za kodi. |
| | kuelezea ukokotoaji wa hesabu za msingi za kodi katika usimamizi binafsi wa fedha. |
| | kuelezea umuhimu wa kutumia wataalamu wa kodi katika kutekeleza sheria na kanuni za kodi. |
| | kuelezea umuhimu na faida za kulipa kodi katika uchumi. |
| | kuelezea aina mbalimbali za kodi zinazohusiana na usimamizi binafsi wa fedha. |
| 3.1.2. Kuelezea wajibu wa kifedha unaohusiana na usimamizi binafsi wa fedha | kuelezea umuhimu wa kutimiza majukumu binafsi ya kifedha. |
| | kuelezea majukumu binafsi ya kifedha (ulipaji wa madeni,kodi, bili, ushuru,malezi, michango ya kijamii). |
| | kuelezea athari za kutotimiza majukumu binafsi ya kifedha. |

| | Vigezo vya tathmini | Mbinu za tathmini | Nyenzo za tathmini |
|---|---|---|---|
| | 2.1.6.1 kuchambua kwa usahihi mchakato wa ukopaji kama unavyotumika katika usimamizi binafsi wa fedha | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 3.1.1.1 kuelezea kwa usahihi wajibu binafsi wa mlipa kodi katika usimamizi binafsi wa fedha. | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 3.1.2.1 kuelezea kwa usahihi majukumu yanayohusiana na usimamizi binafsi wa kifedha. | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |

| **Matokeo Madogo Wezeshi**<br>**Wanafunzi wataweza;** | **Shughuli zinazofanyika** |
|---|---|
| 3.1.3. kuelezea shughuli haramu za kifedha zinazohusiana na usimamizi binafsi wa fedha | kuelezea vitendo haramu vya kifedha (ulaghai, miradi ya upatu haramu, udanganyifu, utakatishaji wa fedha, ufadhili wa ugaidi, kughushi, uhalifu wa kimtandao, uhalifu uliopangwa). |
| | kuelezea umuhimu wa kutojihusisha na vitendo haramu vya kifedha |
| | kuelezea jinsi ya kugundua ishara za vitendo haramu vya kifedha. |
| | kuelezea jinsi ya kujilinda dhidi ya vitendo haramu vya kifedha. |
| | kuelezea njia tofauti za kuripoti vitendo haramu vya kifedha |
| | kuonesha athari za kujihusisha na vitendo haramu vya kifedha. |
| 3.2.1 kuchambua mchakato wa udhibiti binafsi wa vihatarishi vya masuala binafsi ya fedha. | kuelezea umuhimu wa udhibiti wa vihatarishi katika masuala binafsi ya fedha |
| | kutambua vyanzo vya vihatarishi katika usimamizi binafsi wa fedha. |
| | kuonesha ukubwa wa vihatarishi vya kifedha katika mazingira na shughuli tofauti. |
| | kutambua bidhaa na mbinu zinazofaa za kupunguza vihatarishi (mfuko wa dharura, mseto wa uwekezaji, bima, mipango ya fidia, mifuko ya hifadhi ya jamii). |
| | kuelezea maombi yaliyothibitishwa ya teknolojia ya masuala ya kifedha kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa vihatarishi na utoaji wa bidhaa za bima. |

| | Vigezo vya tathmini | Mbinu za tathmini | Nyenzo za tathmini |
|---|---|---|---|
| | 3.1.3.1. kuelezea kwa usahihi vitendo haramu vinavyohusiana na usimamizi binafsi wa fedha. | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 3.2.1.1. kuelezea kwa usahihi mchakato wa udhibiti binafsi wa vihatarishi vya kifedha | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |

| **Matokeo Madogo Wezeshi**<br>**Wanafunzi wataweza;** | **Shughuli zinazofanyika** | |
|---|---|---|
| 3.2.2. kuchambua mchakato wa mipango ya muda mrefu wa masuala binafsi ya kifedha | kuelezea umuhimu wa mipango ya muda mrefu ya masuala binafsi ya kifedha. | |
| | kuelezea bidhaa na huduma mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza mipango ya muda mrefu ya kifedha (akiba ya muda mrefu, uwekezaji, mifuko ya hifadhi ya jamii, bima ya maisha). | |
| | kuchambua faida na hasara za bidhaa na huduma mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza mipango ya muda mrefu ya masuala ya kifedha. | |
| | kuelezea uhusiano kati ya mzunguko wa fedha, vihatarishi na mipango ya muda mrefu ya kifedha. | |
| | kuelezea jinsi ya kuandaa na kufuatilia mipango ya muda mrefu ya kifedha. | |
| | kuelezea uhusiano kati ya kuandaa urithi na wosia katika mipango ya muda mrefu ya kifedha | |
| 3.2.3. kuelezea mchakato wa kuwalinda watumiaji wa huduma za kifedha kama unavyotumika katika masuala binafsi ya kifedha | kuelezea jinsi ya kuwalinda watumiaji wa huduma za kifedha. | |
| | kuonesha umuhimu wa kuwalinda watumiaji wa huduma za fedha. | |
| | kufafanua vihatarishi, haki na wajibu wa watumiaji katika kujihusisha na watoa huduma za fedha. | |
| | kuonesha hatua za kushughulikia na kutatua malalamiko ya watumiaji wa huduma za fedha | |
| | kulezea njia mbalimbali za kuripoti juu ya mwenendo usiofaa wa watoa huduma za fedha. | |
| | kuonesha umuhimu wa kutambua na kuchukua hatua kwa wakati kuhusiana na taarifa na tahadhari kwa watumiaji wa huduma za fedha | |

| | Vigezo vya tathmini | Mbinu za tathmini | Nyenzo za tathmini |
|---|---|---|---|
| | 3.2.2.1 kuchambua kwa usahihi mchakato wa mipango ya muda mrefu katika masuala binafsi ya kifedha | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |
| | 3.2.3.1 kuelezea kwa usahihi mchakato wa kumlinda mtumiaji wa huduma za fedha kama unavyotumika katika masuala binafsi ya kifedha | • mazoezi<br>• mazoezi ya mafunzo kwa vitendo<br>• mitihani | • ripoti za mazoezi<br>• video ya mafunzo kwa vitendo<br>• karatasi ya maswali na mfano wa majibu. |

## Uwekaji wa Viwango vya Vigezo vya Tathmini

Uwekaji wa viwango vya tathmini ni njia ya kutambua mafanikio ya mWanafunzi kulingana na taarifa ambazo zinaonesha kile ambacho mwanafunzi anatarajiwa kufanya ili kuonesha amefanikiwa kufikia matokeo madogo wezeshi. Taarifa hizi zimeundwa kulingana na kazi ambazo mWanafunzi anatarajiwa kufanya ili kupata matokeo husika. Katika mtaala huu, uwekaji wa viwango vya tathmini unajumuisha taarifa ya utendaji inayoonesha vigezo vya kuwapima Wanafunzi katika ngazi za kuridhisha, vizuri, vizuri sana na bora.

Inatarajiwa kwamba wawezeshaji wa moduli wataandaa na kutumia viwango

vya tathmini kwa kila matokeo ya ujifunzaji kwa kutumia mifano iliyo (uk 22)

| Vigezo vya Tathmini | **Vigezo**<br>**Wanafunzi: Ana uwezo wa** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Inaridhisha** | **Vizuri** | **Vizuri Sana** | **Bora** |
| 2.1.1.1. Kuelezea kwa usahihi tofauti kati ya fedha halali na bandia. | kufafanua fedha halali na bandia. | kufafanua fedha halali na bandia.<br><br>kueleza alama za utambuzi wa fedha halali. | kufafanua fedha halali na bandia.<br><br>kueleza alama za utambuzi wa fedha halali.<br><br>kutambua fedha halali na bandia. | kufafanua fedha halali na bandia.<br><br>kueleza alama za utambuzi wa fedha halali.<br><br>kutambua fedha halali na bandia.<br><br>kutumia zana na vifaa katika kutambua fedha halali. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2.1.2.1. kuchambua kwa usahihi mchakato wa fedha zenye ubora kama inavyotumika katika usimamizi wa fedha. | kufafanua fedha zenye ubora. | kufafanua fedha zenye ubora.<br><br>kuelezea sifa za fedha zenye ubora. | kufafanua fedha zenye ubora.<br><br>kuelezea sifa za fedha zenye ubora.<br><br>kuonesha njia sahihi za kutumia na kutunza fedha. | kufafanua fedha zenye ubora.<br><br>kuelezea sifa za fedha zenye ubora.<br><br>kuonesha njia sahihi za kutumia na kutunza fedha.<br><br>kuelezea hatua za kushughulikia fedha zilizoharibika. |

# 14 MAELEZO YA MODULI

## Maelezo ya Moduli ya kwanza

**Msimbo wa Moduli:**
CFE01

**Jina la Moduli:**
Ujuzi wa Hesabu za Kifedha

**Idadi ya hadia:**
1

Matokeo Madogo Wezeshi

**Wanafunzi wataweza;**
- kuonesha ujuzi wa msingi wa hesabu katika masuala binafsi ya fedha.
- kukokotoa viwango vya riba kwenye bidhaa na huduma za fedha.
- Kutumia ujuzi wa hesabu za kifedha kwa ajili ya kufanya uamuzi wa kifedha.

| **Moduli tangulizi :** | Hakuna |
|---|---|

**Muktadha wa Ujifunzaji:**
Moduli hii itafundishwa kupitia mihadhara,uwasilishaji, kazi na mazoezi ya vitendo na majadiliano kwa vikundi

**Nyenzo za ujifunzaji:**
Mkufunzi: Chatipindu, makapeni, vikokotozi, kompyuta na projekta ya LCD.

**Mwanafunzi:**
Vitabu, ripoti za fedha, matukio na fomu za data.

**Mbinu Jumuishi za Tathmini:**

Tathmini Endelevu: 60%

Mtihani wa Mwisho: 40%

## Maelezo ya Moduli ya Pili

**Msimbo wa Moduli:**
CFE02

**Jina la Moduli:**
Mfumo wa Ikolojia ya Kifedha

**Idadi ya hadia:**
1

Matokeo Madogo Wezeshi

**Wanafunzi wataweza;**

- kuelezea kuhusu watoa huduma za fedha kwa masuala binafsi ya kifedha
- kuelezea kuhusu bidhaa na huduma za fedha kwa masuala binafsi ya kifedha
- kuonesha mazingira ya kisheria na usimamizi kwa ajili ya masuala binafsi ya kifedha.
- kuonesha miundombinu wezeshi ya kupata huduma za kifedha kwa ajili ya masuala binafsi ya kifedha

**Moduli tangulizi:**
Hakuna

**Muktadha wa ujifunzaji:**
Moduli hii itafundishwa kupitia mihadhara, uwasilishaji, kazi na mazoezi ya vitendo na majadiliano kwa vikundi.

**Nyenzo za ujifunzaji: Mkufunzi:**
Chatipindu, makapeni, vikokotozi, kompyuta na projekta ya LCD.

**MWanafunzi:**
Machapisho, matukio, sheria, kanuni na miongozo.

**Njia Jumuishi za Tathmini:**
Tathmini Endelevu: 60%

Mtihani wa Mwisho: 40%

## Maelezo ya Moduli ya Tatu

**Msimbo wa Moduli:**
CFE03

**Jina la Moduli:**
Usimamizi wa Fedha

**Idadi ya hadia:**
1

**Matokeo Madogo Wezeshi**

**Wanafunzi wataweza;**

- kutofautisha fedha halali na fedha bandia.
- kuchambua mchakato wa fedha zenye ubora kama unavyotumika katika usimamizi wa fedha
- kuelezea shughuli halali za kuzalisha mapato na maadili ya kazi kulingana na sheria za nchi.
- kuchambua mchakato wa kuweka akiba kama ilivyo katika usimamizi wa fedha.
- kuandaa bajeti na mpango binafsi wa fedha kama ilivyo katika usimamizi wa fedha.

- kuchambua mchakato wa kukopa kama unavyotumika katika usimamizi binafsi wa fedha

**Moduli Tangulizi:**
Hakuna

**Muktadha wa ujifunzaji:**
Moduli hii itafundishwa kupitia mihadhara,uwasilishaji, kazi na mazoezi ya vitendo na majadiliano kwa vikundi.

**Nyenzo za ujifunzaji:**
Mkufunzi: Noti/sarafu za benki, Chatipindu, makapeni, vikokotozi, kompyuta na projekta ya LCD.

**Mwanafunzi:**
Vitabu, vielelezo, matukio na programu za teknolojia ya masuala ya kifedha zilizothibitishwa.

**Njia Jumuishi za Tathmini:**
Tathmini Endelevu: 60%

Mtihani wa Mwisho: 40%

## Maelezo ya Moduli ya Nne

**Msimbo wa Moduli:**
CFE04

**Jina la Moduli:**
Majukumu ya Kifedha

**Idadi ya hadia:**
1

Matokeo Madogo Wezeshi

**Wanafunzi wataweza;**

- kuelezea wajibu binafsi katika kodi unaohusiana na masuala binafsi ya kifedha

- kuelezea wajibu wa kifedha unaohusiana na usimamizi binafsi wa fedha
- kuelezea shughuli haramu za kifedha zinazohusiana na usimamizi binafsi wa fedha

Moduli Tangulizi:
Hakuna

**Muktadha wa ujifunzaji:**
Moduli hii itafundishwa kupitia mihadhara, uwasilishaji, kazi na mazoezi ya vitendo na majadiliano kwa vikundi.
Nyenzo za ujifunzaji: Mkufunzi: Chatipindu, makapeni, vikokotozi, kompyuta na projekta ya LCD.

**Mwanafunzi:**
Machapisho, matukio, sheria, kanuni na miongozo.

**Njia Jumuishi za Tathmini:**
Tathmini Endelevu: 60%

Mtihani wa Mwisho: 40%

## Maelezo ya Moduli ya Tano

**Msimbo wa Moduli:**
CFE05

**Jina la Moduli:**
Ulinzi Binafsi wa Kifedha

**Idadi ya hadia:**
1

## Matokeo Madogo Wezeshi

**Wanafunzi wataweza;**

- kuchambua mchakato wa udhibiti wa vihatarishi vya masuala binafsi ya fedha.
- kuchambua mchakato wa mipango ya muda mrefu ya masuala binafsi ya kifedha
- kuelezea mchakato wa kuwalinda watumiaji wa huduma za kifedha

kama unavyotumika katika masuala binafsi ya kifedha

**Moduli Tangulizi:**
Hakuna

**Muktadha wa ujifunzaji:**
Moduli hii itafundishwa kupitia mihadhara,uwasilishaji, kazi na mazoezi ya vitendo na majadiliano kwa vikundi.

**Nyenzo za ujifunzaji: Mkufunzi:**
Chatipindu, makapeni, vikokotozi, kompyuta na projekta ya LCD.
MWanafunzi: Machapisho, matukio, sheria, kanuni na miongozo. .

Njia Jumuishi za Tathmini:
Tathmini Endelevu: 60%
Mtihani wa Mwisho: 40%

# WADAU WA MSINGI

Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar.fisi ya Rais, Kazi, Masuala ya Uchumi na Uwekezaji, Zanzibar.Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.Wizara ya Fedha.

Wizara ya Viwanda na Biashara.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Zanzibar

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar

Benki Kuu ya Tanzania.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

Bodi ya Bima ya Amana.

Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania.

Umoja wa Benki Tanzania

Umoja wa Kampuni za Simu Tanzania

Umoja wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha, Tanzania (TAMFI)

Umoja wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha, (wasiochukua amana) Tanzania (TAMIU)

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Chama cha Kutetea Haki za Walaji Tanzania

Umoja wa Kampuni za Bima Tanzania

Kamati ya Wanawake ya Huduma Jumuishi za Fedha

# MAREJELEO

1. Balestra, C. and R. Tonkin (2018). "Inequalities in household wealth across OECD countries: Evidence from the OECD Wealth Distribution Database."

2. Bank of Tanzania (Financial Consumer Protection) Regulations, 2019. https://www.bot.go.tz/Publications/Acts,%20Regulations,%20Circulars,%20Guidelines/Regulations/en/2020031802343226.pdf

3. Enache, S., et al. (2023). "Savings or Investment. Personal Budget Management." EIRP Proceedings 18(1): 302-313.

4. Fanta, A., & Mutsonziwa, K. (2021). Financial literacy as a driver of financial inclusion in Kenya and Tanzania. Journal of Risk and Financial Management, 14(11), 561.

5. Financial Sector Deepening Tanzania (FinScope Survey Tanzania), 2023. https://www.fsdt.or.tz/about-us/

6. Hamid, F. S. and Y. J. Loke (2021). "Financial literacy, money management skill and credit card repayments." International Journal of Consumer Studies 45(2): 235-247.

7. Koomson, I., Ansong, D., Okumu, M., & Achulo, S. (2023). Effect of financial literacy on poverty reduction across Kenya, Tanzania, and Uganda. Global Social Welfare, 10(1), 93-103.

8. Kozup, J. and J. M. Hogarth (2008). Financial literacy, public policy, and consumers' self-protection—more questions, fewer answers, Wiley Online Library. 42: 127-136.

9. Lotto, J. (2020). Understanding sociodemographic factors influencing households' financial literacy in Tanzania. Cogent Economics & Finance, 8(1), 1792152.

10. National Council for Financial Inclusion (National Financial Inclusion Framework – III) 2023-2028.


11. OECD, K. (2018). OECD science, technology and innovation outlook 2018, OECD publishing Paris.

12. Robert, K. A., et al. (2013). "Examining the levels of financial literacy and outreach of microfinance institutions in Uganda." Journal Issues ISSN 2350: 157X.

13. Sanderson, A., et al. (2018). "A review of determinants of financial inclusion." International Journal of Economics and Financial Issues 8(3): 1.

14. Stephen, K., Raphael, G., & Shayo, F. (2022). Financial Literacy and Financial Inclusion in Rungwe, Mbeya-Tanzania. The Int Rev Eco Stu: TIRES-106.






# TUNAWATAKIA KILA LA KHERI



# MTAALA WA WAELIMISHAJI WALIOTHIBITISHWA WA ELIMU YA FEDHA

BARAZA LA TAIFA LA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA
TANZANIA 2023